TANGAZO LA SERIKALI Na. 858 la tarehe 11/10/2024

SHERIA YA BENKI KUU YA TANZANIA,
(SURA YA 197)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 28(2) na (3))*

NOTISI YA KUONDOA KWENYE MZUNGUKO NOTI ZA ZAMANI ZA SHILINGI ZILIZOTOLEWA KUANZIA MWAKA 1985 HADI 2003 NA NOTI YA SHILINGI MIA TANO ILIYOTOLEWA MWAKA 2010, YA MWAKA 2024

Jina

**1**. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kuondoa kwenye Mzunguko Noti za Zamani za Shilingi Zilizotolewa Kuanzia Mwaka 1985 hadi 2003 na Noti ya Shilingi Mia Tano Iliyotolewa Mwaka 2010 ya Mwaka 2024.

Kuondoa kwenye mzunguko noti za zamani

**2.** Benki Kuu ya Tanzania inaitisha noti za shilingi kwa malipo halali sawa na thamani zilizotolewa kuanzia mwaka 1985 hadi 2003 na noti ya Shilingi mia tano toleo la mwaka 2010 zenye alama kuu kama ilivyoainishwa katika Jedwali.

Zuio kwa benki kutoa noti zilizoondolewa kwenye mzunguko

**3.** Kuanzia tarehe ya kutangazwa kwa Notisi hii, Benki zote hazitalipa noti zilizotolewa kwenye mzunguko na Benki Kuu ya Tanzania kama ilivyoainishwa katika Jedwali ambazo ni noti za Shilingi ishirini, mia mbili, mia tano, elfu moja, elfu mbili, elfu tano na elfu kumi kwa matoleo ya mwaka 1985 hadi mwaka 2003, na noti ya Shilingi mia tano iliyotolewa mwaka 2010.

Kupokea noti zilizoondolewa kwenye mzunguko

**4**. Kuanzia tarehe 06 Januari, 2025 hadi tarehe 05 Aprili, 2025, Benki Kuu ya Tanzania na benki zote zitakubali amana au maombi ya kubadilisha noti

zilizotolewa kwenye mzunguko na Benki Kuu ya Tanzania kama zilivyobainishwa katika Notisi hii.

Kusitisha matumizi ya noti zilizoondolewa kwenye mzunguko


**5**. Noti zilizoainishwa katika Jedwali zitakoma kuwa fedha halali kuanzia tarehe 06 Aprili, 2025, ambapo benki zote hazitalipa wala kupokea amana au maombi ya kubadilisha noti zilizoondolewa kwenye mzunguko.

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA • THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE


**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

NOTI ZILIZOONDOLEWA KWENYE MZUNGUKO

| NA | KIWANGO KWA SHILINGI | MWAKA WA TOLEO | MAELEZO KUHUSU MUONEKANO WA NOTI | PICHA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 20 | 1985 | Rangi: Zambarau.<br><br>Mbele: Mwenge wa Uhuru, Nembo ya Taifa, Rais wa kwanza, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.<br><br>Nyuma: Mfanyakazi na mashine katika kiwanda cha tairi, ramani ya Tanzania bila visiwa, Utepe wa usalama.<br><br>Alama iliyofichika: kichwa cha Twiga. |     |
| 2. | 20 | 1986 | Rangi: Zambarau.<br><br>Mbele: Mwenge wa Uhuru, Nembo ya Taifa, Rais wa kwanza, Mwalimu |   |

*Tangazo la Serikali Na.858 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Julius Kambarage Nyerere.<br><br>Nyuma: Mfanyakazi na mashine katika kiwanda cha matairi, ramani ya Tanzania yenye visiwa, Utepe wa usalama.<br><br>Alama iliyofichika: Kichwa cha Twiga. |  |
| 3. | 20 | 1987 | Rangi: Zambarau.<br><br>Mbele: Mwenge wa Uhuru, Nembo ya Taifa, Rais wa Awamu ya pili Ali Hassan Mwinyi.<br><br>Nyuma: Wafanyakazi na mashine katika kiwanda cha matairi, ramani ya Tanzania yenye visiwa, Mwenge wa Uhuru, Utepe wa usalama.<br><br>Alama iliyofichika: Kichwa cha Twiga. | <br> |
| 4. | 200 | 1986 - 1992 | Rangi: Kahawia, hudhurungi na chungwa. |  |

*Tangazo la Serikali Na.858 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Mbele: Mwenge wa Uhuru, Nembo ya Taifa, Rais wa Awamu ya pili Ali Hassan Mwinyi.<br><br>Nyuma: Wanaume wawili katika maji yenye kina kifupi wakiwa na samaki, mashua, ramani ya Tanzania yenye visiwa, mwenge wa uhuru, Utepe wa usalama,<br><br>Alama ya iliyofichika: Kichwa cha Twiga. |  |
| 5. | 200 | 1993 – 1995 | Rangi: Kahawia, hudhurungi na chungwa.<br><br>Mbele: Chui mwenye watoto wawili, Nembo ya Taifa, Rais wa Awamu ya pili Ali Hassan Mwinyi.<br><br>Nyuma: Wanaume wawili katika maji yenye kina kifupi wamebeba samaki, boti, ramani ya Tanzania yenye visiwa, Utepe wa usalama.<br><br>Alama iliyofichika: Hakuna. |  |

*Tangazo la Serikali Na.858 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 6. | 500 | 1990 | Rangi: bluu, waridi na chungwa.<br><br>Mbele: Pundamilia, Nembo ya Taifa, Rais wa Awamu ya pili Ali Hassan Mwinyi.<br><br>Nyuma: Mwanamke aliyeketi na kikapu, wafanyakazi watano wakivuna karafuu, matunda ya kahawa, Utepe wa usalama,<br><br>Alama iliyofichika: kichwa cha Twiga. |  |
| 7. | 500 | 1993 – 1995 | Rangi: Zambarau, kijani na chungwa.<br><br>Mbele: Pundamilia, Nembo ya Taifa, Rais wa Awamu ya pili Ali Hassan Mwinyi.<br><br>Nyuma: Mwanamke aliyeketi na kikapu na wafanyakazi watano wakivuna karafuu, matunda ya kahawa, Mwenge wa Uhuru, Utepe wa usalama uliochapwa maneno "BENKI |  |

*Tangazo la Serikali Na.858 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | KUU YA TANZANIA".<br><br>Alama iliyofichika: kichwa cha Twiga. | |
| 8. | 500 | 1997 | Rangi: Zambarau, kijani na chungwa.<br><br>Mbele: Pundamilia, Nembo ya Taifa, Rais wa Awamu ya pili Ali Hassan Mwinyi.<br><br>Nyuma: Mwanamke aliyeketi na kikapu, wafanyakazi watano wakivuna karafuu, matunda ya kahawa, Utepe wa usalama uliochapwa maneno "BENKI KUU YA TANZANIA".<br><br>Alama iliyofichika: Kichwa cha Twiga. |  |
| 9. | 500 | 2003 | Rangi: Kijani.<br><br>Mbele: Nembo ya Taifa, Nyati, Miti, Utepe wa Usalama wenye maandishi |  |

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA · THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ya rangi ya fedha 'BOT 2003'.<br><br>Nyuma: Mashua, Jengo la ukumbi mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Nyoka aliyejiviringisha kwenye fimbo, Twiga.<br><br>Alama iliyofichika: Kichwa cha Twiga na maandishi maalumu 500. |  |
| 10. | 500 | 2010 | Rangi: Kijani.<br><br>Mbele: Nembo ya Taifa, Picha ya Sheikh Abeid Aman Karume Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Utepe wa usalama wenye mawimbi yanayaonekana pale noti hiyo inapogeuzwageuzwa upande au juu na chini.<br><br>Nyuma: Nyoka aliyeviringishwa kwenye fimbo, Jengo la ukumbi mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wanafunzi waliohitimu wakiwa wamevaa kofia na gauni za mahafali. | <br> |

*Tangazo la Serikali Na.858 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Alama iliyofichika: Sura ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na maandishi maalumu 500. | |
| 11. | 1000 | 1990 | Rangi: Kijani, zambarau na kutu.<br><br>Mbele: Tembo na mtoto wake, Nembo ya Taifa, Rais wa Awamu ya Pili Ali Hassan Mwinyi.<br><br>Nyuma: majengo ya kiwanda, Mmea, mlango wa kale wenye nakshi wa Jengo la Benki ya Watu wa Zanzibar, Utepe wa usalama uliochapishwa maneno BENKI KUU YA TANZANIA.<br><br>Alama iliyofichika: Kichwa cha Twiga. |  <br>  |
| 12. | 1000 | 1993 - 1995 | Rangi: Kijani, kahawia na nyekundu.<br><br>Mbele: Tembo na mtoto wake, Nembo ya Taifa, |   |


*Tangazo la Serikali Na.858 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Picha ya Rais wa Awamu ya pili Ali Hassan Mwinyi.<br><br>Nyuma: Majengo ya kiwanda, Mmea, Mlango wenye nakshi wa Benki ya Watu wa Zanzibar, Utepe wa usalama uliochapishwa maneno BENKI KUU YA TANZANIA.<br><br>Alama iliyofichika: Kichwa cha Twiga. |  |
| 13. | 1000 | 1997 | Rangi: Kijani, kahawia na nyekundu.<br><br>Mbele: Tembo wawili, Nembo ya Taifa, Picha ya Rais wa Awamu ya pili wa Tanzania Ali Hassan Mwinyi.<br><br>Nyuma: Majengo ya kiwanda, mimea, mlango wa kale wenye nakshi wa Benki ya Watu wa Zanzibar, Utepe wa usalama uliochapishwa maneno BENKI KUU YA TANZANIA.<br><br>Alama iliyofichika: |  |

*Tangazo la Serikali Na.858 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Kichwa cha Twiga. | |
| 14. | 1000 | 2000 | Rangi: Kijani, kahawia na nyekundu.<br><br>Mbele: Tembo wawili, Nembo ya Taifa, Rais wa kwanza wa Tanzania Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.<br><br>Nyuma: Majengo ya kiwanda, Mmea, mlango wa kale wenye nakshi wa Jengo la Benki ya Watu wa Zanzibar, Utepe wa usalama uliochapishwa maneno BENKI KUU YA TANZANIA.<br><br>Alama iliyofichika: Kichwa cha Twiga. |     |
| 15. | 1000 | 2003 | Rangi: Zambarau.<br><br>Mbele: Nembo ya Taifa, Picha ya Rais wa Awamu ya Kwanza wa |   |

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA · THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Tanzania Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Jiwe la Bismark lililopo bandarini Mwanza, utepe wa holographic wenye tarakimu 1000.<br><br>Nyuma: Jengo la Ikulu ya Dar es Salaam juu yake ikipepea Bendera ya Rais, Mimea, utepe wa usalama wenye Maneno BOT 2003.<br><br>Alama iliyofichika: Kichwa cha Twiga na maandishi maalumu ya 1000. |  |
| 16. | 2000 | 2003 | Rangi: Hudhurungi na kahawia.<br><br>Mbele: Nembo ya Taifa, Picha ya Simba na Mlima Kilimanjaro, utepe wa holographic wenye tarakimu 2000.<br><br>Nyuma: Ngome Kongwe, mawe ya mviringo, Utepe wa usalama wenye maandishi ya metali BOT 2003.<br><br>Alama iliyofichika: Kichwa cha Twiga |  |

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA

*Tangazo la Serikali Na.858 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | na maandishi maalumu ya 2000. | |
| 17. | 5000 | 1993 | Rangi: Kahawia na njano.<br><br>Mbele: Nembo ya Taifa, Picha ya Rais wa Awamu ya pili wa Tanzania Ali Hassan Mwinyi, Kifaru, utepe wa usalama.<br><br>Nyuma: Twiga sita, Mlima Kilimanjaro na kasha.<br><br>Alama iliyofichika: Kichwa cha Twiga. | <br> |
| 18. | 5000 | 1997 | Rangi: Kahawia na njano.<br><br>Mbele: Kifaru, Nembo ya Taifa, Kichwa cha Twiga, alama ya usalama yenye maandishi maalumu BOT 5000.<br><br>Nyuma: Twiga sita, Mlima Kilimanjaro, kasha.<br><br>Alama iliyofichika: Kichwa cha Twiga. | <br> |

*Tangazo la Serikali Na.858 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 19. | 5000 | 2003 | Rangi: Zambarau.<br><br>Mbele: Nembo ya Taifa, Kifaru mweusi na mawe. utepe wa holographic wenye tarakimu 5000.<br><br>Nyuma: Nyumba ya maajabu iliyopo Zanzibar, mtambo wa kuchimba madini, Utepe wa usalama wenye maandishi maalumu BOT 2003.<br><br>Alama iliyofichika: Kichwa cha Twiga na maandishi maalumu ya 5000. | <br> |
| 20. | 10000 | 1993 - 1995 | Rangi: Bluu na nyekundu.<br><br>Mbele: Simba, Nembo ya Taifa, Picha ya Rais wa Awamu ya pili wa Tanzania Ali Hassan Mwinyi, Utepe wa usalama.<br><br>Nyuma: Jengo la zamani la Benki ya Tanzania, Jengo la Nyumba ya Maajabu lililopo Zanzibar.<br><br>Alama iliyofichika: Kichwa cha Twiga. | <br> |

*Tangazo la Serikali Na.858 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 21. | 10000 | 1997 | Rangi: Bluu na Nyekundu.<br><br>Mbele: Simba, Nembo ya Taifa, Kichwa cha Twiga, utepe wa holographic,<br>Utepe wa usalama wenye maandishi maalumu “BOT 10000”.<br><br>Nyuma: Jengo la Benki ya Tanzania, Jengo la Nyumba ya Maajabu lililopo Zanzibar.<br><br>Alama iliyofichika: Kichwa cha Twiga. | <br> |

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

*Tangazo la Serikali Na.858 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 22. | 10000 | 2003 | Rangi: Nyekundu na njano.<br><br>Mbele: Nembo ya Taifa, Tembo, utepe wa holographic, wenye tarakimu 10000.<br><br>Nyuma: Jengo la Benki Kuu Dar es Salaam, Bwawa la maji yanayotiririka, maua, utepe wa usalama wenye maandishi maalumu BOT 2003.<br><br>Alama iliyofichika: Kichwa cha Twiga na maandishi maalumu ya 10000. | <br> |

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

Dodoma,
10 Oktoba, 2024

EMMANUEL M. TUTUBA,
*Gavana*